Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 4, Issue 3

13th Dhul-Hijjah 1431

19th November, 2010

Yaliyomo

Chanzo Cha Shirk 1 – 2

Hukmu Zenye Kuhusiana Na 'Idd 2 – 4

CHANZO CHA SHIRK

Mtayarishi: Imaam Muhammad Naasirud-Deen al-Albaani

Kutokamana na yale yaliyo thubutu katika sheria ya dini ni kuwa wana-adamu walikuwa - hapo awali - ummah mmoja ulio juu ya Tawheed ya sawa, baadae Shirk ikawashinda pole pole. Alieyasema haya ni Allaah Mwingi wa Rehma AliyeTukuka : **"Wanadamu wote walikuwa ni ummah mmoja, Allaah akatuma manabii wakaleta bishara njema na kuwaonya.** (al Baqarah 2:213)

Ibn Abbas (رضي الله عنه) amesema: "Baina ya Nuh na Adam kulikuwemo vizazi kumi, vyote vilikuwa juu ya sheria ya haki, baadaye wakafarikiana. Basi Allaah akatuma manabii wenye kuleta bishara njema na kuwaonya" [2]

Ibn 'Urwah al-Hanbalee (837 H) akasema: "Maneno haya yanawakanusha wana historia kutoka Ahlul Kitaab (yaani Mayahudi na Manasara) waliodai kuwa Qaabil (Cain) na kizazi chake walikuwa wakiabudu moto." [3]

Nami nasema: Ndani ya maneno haya ni ukanushaji wa baadhi ya wana filosofia (philosophers) na makafiri (wasioamini Mungu) wanao dai kuwa asili ya chanzo cha mwanadamu ni Shirk, na Tawheed ni yenye kukulia na mwanadamu (evolved). Aayah iliotangulia inakadhibisha dai lao, na vile vile hadithi hizi mbili zifuatazo:

Kwanza: Aliposema Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa Allaah (عز وجل) Amesema): **"Niliwaumba waja wangu wote juu ya dini ya haki (juu ya Tawheed, mbali na Shirk). Baadaye mashetani wakawajia na kuwapotosha kutokamana na dini hio yao ya haki. Wakawafanyia kuwa ni halali yale Niliyowafanyia haramu, na wakawaamrisha kunishirikisha mimi katika 'ibaadah, (haya ni) katika mambo ambayo sikuwaamrisha."** [4]

Pili: Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: *"Kila mtoto huzaliwa juu ya fitrah* **[5],** *lakini wazazi wake humfanya awe ni myahudi, au mnasara au majusi. Ni mfano wa mnyama anapozaa kizazi cha kawaida, jee mumewahi kuona mnyama aliyezaliwa ilhali amelemaa, kabla ya nyinyi kuwalemaza?"* Abu Hurayrah akasema: Soma kwa hiari yako: **"Fitrah ambayo Allaah alilo waumbia watu. Hakuna mabadiliko katika uumbaji wa Allaah. "** (Surat Roum 30:30) [6]

Baada ya hii kielezo kilicho wazi, ni katika mambo muhimu zaidi kwa muislamu kujua namna Shirk inavyoenea baina ya waumini, baada ya kuwa muwahhideen (ummah walioshikamana na Tawheed). Kuhusiana na msemo wa Allah -aliye Mkamilifu - juu ya watu wa Nuh: **"Na walisema: msiwawache miungu yenu, wala msimwache Wadda, wala Suwaa, wala Yaghutha, wala Nasra"** (Suratul Nuh 71:23)
Imenukuliwa na kundi miongoni mwa salaf (watangulizi wetu wema), kuwa, katika misemo mengi hawa miungu watano walikuwa ni watu wema. Lakini, walipokufa, shetani akanong'oneza baina ya watu kuenda faragha katika makaburi yao. Kisha shetani akawanong'ona waliokuja baada yao kuwa wawafanye miungu huku akiwapambia (katika mnong'ono) wazo la kuwa (huko kuwafanyia masanamu watu hao wema) utawafanya wao kuwakumbuka na kuwaiga katika kutenda mema. Baadaye shetani akawashauri kizazi cha tatu kilichofuatia kuwa wawaabudu hao masanamu pamoja na Allah Aliyetukuka - na akawanong'oneza kuwa hili ni jambo wazee wao wa kale walikuwa wakilifanya.
Basi Allaah akawatumilizia wao nabii Nuh, kuwaamrisha wamuabudu Allaah peke yake. Walakini hakuna aliye itika mwito wake isipokuwa wachache. Allaah aliyeTukuka ametunukulia kisa hichi chote katika Surat -Nuh. Ibn Abbas akasema: "Kwa hakika haya majina matano ya watu wema ni katika watu wa Nuh. Walipokufa, shetani aliwanong'oneza watu wao ili watengeneze sanamu za watu hao na kuziweka mahali pa mkutano ili uwe ukumbusho. Nao wakafanya hivo. Walakini, hamna miongoni mwao aliye abudu masanamu hayo.Mpaka walipofariki, dhamira ya masanamu hayo ikasahaulika. Baadaye kizazi kilichofuatia ndio wakaanza kuyaabudu (masanamu hayo)" [7]

Mifano ya haya imenukuliwa pia na Ibn Jareer na wengineo, kutoka kwa ma salaf (wengi) radhi za Allaah ziwafikie. Katika kitabu cha ad-Durral-Manthoor (6/269): Abdullah ibn Humaid akatuhadithia kutoka kwa Mutahhar, ambaye aliesema: Yazeed ibn al-Muhallab alitajwa kwa Abu Ja'far al Baaqir (11H), naye akasema: Aliuwawa pahali ambapo mwengine asiyekuwa Allaah alikuwa akiabudiwa. Kisha akamtaja Wadd na akasema: "Wadd alikuwa ni muislamu aliyependwa mno na watu wake. Alipokufa, watu wake wakaanza kukusanyika katika kaburi lake huko bara la Baabil (Babel), huku wakiomboleza. Iblees (Shetani) alipowaona wakihuzunika na kuomboleza juu yake, alijigeuza katika

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

CHANZO CHA SHIRK

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

sura za binadamu na akawatokea na kusema "Naona kuwa munaomboleza juu yake (yaani Wadd). Kwa nini musitengeneze sanamu yake na kuiweka mahali munapo kusanyika; jambo ambalo litawakumbusha (Wadd). Nao wakaitika shauri hilo na kutengeneza picha (sanamu) yake na kuiweka maskani yao wanapokusanyika, jambo ambalo lilifanya wamkumbuke Wadd. Iblees alipowaona wanamkumbuka kupindukia mipaka, akawaambia: "Ni kwa nini basi kila mmoja wenu asitengeneze sanamu mfano huo na kuiweka majumbani mwenu, ili kila mara mutamkumbuka" Nao wote wakaitika "Naam". Kila nyumba ikawa na picha (sanamu) yake, ambayo waliipenda na kuitukuza na ambayo kila mara iliwakumbusha juu yake. Abu Ja'afar akasema: "Wale waliokuja katika kizazi kilichofuatia waliona jinsi kizazi kilichotangulia walichokifanya, nakulizingatia jambo hilo.....kufikia kiasi yakumfanya kuwa ni mungu wakuabudiwa pamoja na Allaah. Akaendelea kusema: Hii ndio ilikuwa sanamu ya kwanza kufanyiwa ibada badala ya Allaah, na wakaliita sanamu hilo 'Wadd'. [8]

Ndio katika hikma zake Allaah - Mwingi wa Rehma aliye Tukuka - alivyotekeleza, alipomtumilisha Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kuwa ni mjumbe wa mwisho na kuifanya sheria yake kuwa ni utimizo wa hukmu zake tukufu, ndani yake Allaah akakataza njia zote ambazo watu wanaweza angukia kwenye Shirk - ambayo ni dhambi kubwa kushinda zenginezo. Yote haya huelekeza katika kupindukia mipaka na huongoza katika ibada ya asiyekuwa Allaah aliye Tukuka.
Hii ndio hali ilivyo, hasa katika zama ambazo ilimu ni yenye kudidimia, na ujinga unazidi, kuna wachache wenye kutoa nasiha (ya haki na ukweli) na Shetani anashirikiana na binadamu na majini ili kuwapotosha watu na kuwapurukusha katika kumwabudu Allaah pekee yake - mwingi wa Rehma aliye Tukuka.

<u>KUMBUKUMBU</u>:

1. Tahdheerus Saajid min Ittikhadil Qubouri Masaajid (Uk. 101 -106)

2. Imenukuliwa na Ibn Jabeer at Tabaree katika tafsiri yake (4/275) na al-Haakim (2/546) ambaye alisema: "Ni sahih kulingana na mizani ya Bukhari". Adh-Dhahabee alikubaliana naye.

3. Al-Kawaakibud Duraaree fee Tarteeb Musnad Imaam Ahmad 'alaa Abwaabil Bukharee. (6/212/1)

4. Imepokewa na Muslim (8/159) na Ahmad (4/162) kutokamana na Iyadh ibn Himaar al-Mujaashi'ee (R.A)

5. Ibn al-Atheer asema katika an-Nihaayah (3/457) "al-Fitr": maana yake ni kuanzisha kuumba, na al-Fitrah ni hali inayotokamana na hayo. Maana yake ni kuwa, binadamu anazaliwa katika hali ambayo yuko tayari kukubali dini ya haki. Basi akiwachwa juu ya haya naye ataendelea kushikamana na dini ya haki. Walakini, wale wanao yabadilisha hayo, hufanya hivo kwa ajili ya udhaifu wa binadamu na kufuata bila ya kuzingatia. Al-Haafidh Ibn Hajar alisema katika al-Fath (3/248): "Watu hutofautiana juu ya maana ya neno al-fitrah, na msemo mashuhuri ni kuwa inamaanisha Uislamu. Ibn 'Abdul Barr akasema: Hilo ndilo lenye kutambulika zaidi miongoni mwa ma salaf, na wanavyuoni wa tafsiri wanakubaliana kuwa kile kilicho kusudiwa na maneno ya Allaah alie Tukuka" Fitra ya Allaah aliyewaumbieni wanadamu" ni Uislamu.

6. Imepokewa na Bukhari (11/148) na Muslim (18/52)

7. Imepokewa na Bukhari.

8. Imepokewa na Ibn Haatim, katika al-Kawaakibud-Duraaree (6/112/2) ya Ibn 'Urwa al-Hanbalee, pamoja na Isnaad ilio Hasan, mpaka Abu Muttahar. Walaakin, hamna wasifu (biography) ilopatikana yake yeye, wala ndani ya kitabu cha al-Kunaa wal-Asmaa cha ad-Dawlabee, wala kitabu cha al-Kunaa cha Muslim, wala cha mtu yeyote mwengine. Na udhaaifu uliofichika hapa ni kuwa mtu huyu ni m-Shee'ah, lakini wasifu haipo katika al-Kunaa ya at-Toosee kutoka kwenye maelezo ya ki Shee'ah.

Hukmu Za 'Idd

[Endelea kutoka Vol. 4; Issue 2]

Hukmu yake ni waajib kulingana na wengi, kwani yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwaamrisha peke yake watu wake wote kwa ujumla;

"... Kwahivyo aliwaamrisha wao wafungue saumu zao, na watoke kwenda kwenye musalla ..."

Hata Mtume (صلى الله عليه وسلم) pia aliwaamrisha makhsusi wanawake wote wakahudhurie; akasema Umm 'Atiyyah;

Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) alituamrisha yakwamba wanawake wakuu na wanawali watoke na kuelekea, isipokuwa tu wanawake walio kwenye heidh wajitenge na musalla;

Na katika riwaya nyengine;

"(Aliamrisha) yakwamba wanawake wakuu na wanawali na watoke kuelekea, isipokuwa walio kwenye heidh (miongoni mwao) na wajitenge na musalla."

Amesema Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله): "Kwahiyo, sisi twajitegemeza kwenye maneno yakwamba *Swalaatul 'Idd* ni waajib kwa kila mtu (*al-'ayn*) kama alivyosema Abu Haneefah na wengineo. Huu ni mmojawapo wa misemo iliyopokewa kutoka kwa ash-Shaafi'ee na mmojawapo wa misemo miwili katika *madh-hab* ya Ahmad. Na inavyosemekana yakwamba si waajib inaonekana kuwa mbali na na ukweli, kwa sababu ni miongoni mwa alama kubwa za Uislamu, na watu wengi hujitokeza kuhudhuria kuliko swala ya Ijumaa. Na *takbeer* imehukumiwa itekelezwe (kuihusu aya). Na kusemekana yakwamba ni faradh kifaayah hakuna msingi ..."

Akasema Ash-Shawkaani: "Jua

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

Hukmu Zenye Kuhusiana Na ‘Idd

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliitekeleza swala hii katika kila siku ya ‘Idd na wala hakuwahi kuiwacha, na akawaamrisha watu wajitokeze kwa wingi wakaihudhurie, hata aliwaamrisha wanawake wakuu, wanawali, na wanawake walio kwenye ada zao za kila mwezi wakahudhurie, akawaambia walio kwenye heidh wasiwe ni wenye kuswali, lakini wahudhurie tu kwenye ‘amali hii nzuri kwa maombi pamoja na Waislamu wenzao. Hata Mtume (صلى الله عليه وسلم) pia akamuamrisha mwanamke ambae aliyekosa *Jilbaab* akaazime kutoka kwa rafikiye. Na yote hayo yanathibitisha yakwamba swala hii ni waajib juu ya kila mtu na wala sio *kifaayah,* na amri ya kutoka na kuelekea kwenye musalla imebaki licha ya kufutwa kwa amri ya kuswali kwa mwenye udhuru wa kutoswali...”. Kisha akasema, “Na miongoni mwa dalili yakwamba ni waajib ni kwamba inaifuta hukmu ya swala ya Ijumaa zinapopambana (siku) zote mbili katika siku moja. Na lisilokuwa ni waajib haliwezi kufuta lile ambalo ni...”

Katika kuisherehesha hadeeth ya Umm ‘Atiyyah, Sheikh al-Albaani (رحمه الله) amesema: “Amri iliyotajwa hapa ni ushuhuda yakwamba ni waajib, na inapokuwa ni waajib kutoka na kwenda kwa ajili yake, basi inakuwa ni waajib kuiswali kwa mwenye kupaswa kuswali ...

WAKATI WA KUISWALI SWALA YA ‘IDD

Kuhusu ‘*Idd ul-Fitr* na ‘*Idd ul-Adh-ha*, swahaba ‘Abdullaah Bin Busheer (رضي الله عنه) amesema; “Tulikuwa tukimaliza kuswali wakati wa tasbeeh.”

Akasema Ibn al-Qayyim; “Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiichelewesha swala ya ‘*Idd ul-Fitr* na alikuwa ni mwenye kuiharakisha swala ya *al-Adh-ha*.na Ibn ‘Umar, ambaye ni shahidi aliyekuwa akiifuata Sunnah hii, alikuwa hatoki kuelekea kwenye musalla mpaka jua lichomoze.”

Siddeeq Hassan Khan amesema: “Wakati wake ni baada ya jua kufikia kimo cha mkuki mpaka katikati ya mchana, na wakati huu unaafikiana na hadeeth, na kwa vile hakuna hoja yenye kueleza mwisho wa wakati wake, basi ni katikati ya mchana.”

Abu Bakr al-Jazaa’iree akasema; “(Wakati wake ni) kuanzia kuchomoza kwa jua kiasi cha kimo cha mkuki mpaka katikati ya mchana. Ingawaje ni bora kuswali *al-Adh-ha* kwenye wakati wake wa mapema ili kuwarahisishia watu wende wakachinje wanyama wao. (Na ni bora) kuichelewesha *Swalatul-Fitr*, ili watu wapate wakati watoke kwenda kugawa *Sadaqaat* zao.”

IWAPO HABARI ZA KUONEKANA KWA MWEZI ZITACHELEWA KUWAFIKIA

Ikiwa haijulikani yakwamba siku ya ’Idd imeingia mpaka baada ya wakati wa swala ya ’Idd, basi swala itaswaliwa siku ifuatayo kulingana na hadeeth swaheeh; “Baadhi ya wasafiri walikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakishuhudia yakwamba wameuona mwezi katika siku iliyotangulia, kwahivyo akawaamrisha (watu) wafungue saumu zao na wende kwenye musalla zao, siku (ya pili) iliyofuata.”

HAKUNA *ADHAAN* WALA *IQAAMAH* KATIKA SWALA ZA ’IDD

Kutoka kwa Jaabir Bin Samurah (رضي الله عنه); “Niliwahi kuswali Swala za ‘Idd pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم), (zaidi ya mara moja) bila ya kuwa na *adhaan* wala *iqaamah*.

Ibn ‘Abbaas na Jaabir (رضي الله عنهما) wamesema: “Hakukuwa na adhaan katika siku ya fitr wala siku ya adh-ha.”

Akasema Ibn al-Qayyim; “Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiwasili katika musalla na kuanza swala bila ya adhaan au iqaamah. Wala hakuwa akisema, ’Swalaatul Jaami’ah’. Sunnah ni kutofanya kitu chochote kama hicho.”

Amesema Sheikh al-Albaani (رحمه الله): “Na ni dalili yakwamba sharee’ah imeyawacha hayo kwenye *Swalaatul ‘Idd*. Kwahivyo, (iwapo yatafanywa kwenye *Swalaatul ‘Idd*), basi hayo yatakuwa ni Uzushi.”

KHUTBAH ZA ’IDD

Sunnah ya khutba za ’Idd ni kwamba hutolewa baada ya swala.

Amesema Ibn ’Abbaas (رضي الله عنهما): “Nilihudhuria swala ya ’Idd pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) ,Abu Bakr, ‘Umar na Uthmaan (رضي الله عنهم), na wote walikuwa wakiswali kabla ya khutbah.”

Akasema Ibn ‘Umar (رضي الله عنه): “Mtume (صلى الله عليه وسلم), Abu Bakr, na ‘Umar waliswali swala za ‘Idd kabla ya khutbah.”

Kuswali kabla ya khutbah ndiyo iliyokuwa Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na *ma-khulafaa* waongofu (رضي الله عنهم), na watu hawakuibadilisha mila hii mpaka baadae. Amesema Abu Sa’eed al-khudhree (رضي الله عنه): “Katika siku ya ‘Idd ul-Adh-ha, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikwenda katika musalla, na jambo la kwanza alilofanya baada ya kufika ilikuwa ni kuswali, kisha baada ya kuikamilisha swala akasimama mbele ya watu, haliyakuwa watu wamekaa kwenye swafu zao. Akawahutubia, akawanasihi, na akawaamrisha. Baada ya hapo, akipenda kutuma kikosi cha jeshi kwenda sehemu fulani, hufanya hivyo, au iwapo akipenda kuamrisha jambo hufanya hivyo, na kisha huondoka akenda zake. Watu wakaandama Sunnah hiyo mpaka nikatoka kuelekea mimi na Marwaan, ameer wa

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Madeenah, kwenda kuswali swala ya '*Idd ul-Adh-ha* au '*Idd ul-Fitr*. Tulipofika kwenye musalla, kulikuwa na minbar iliyotengezwa na Katheer Bin as-Salt. Marwaan akataka kupanda kwenye minbar kabla ya swala. Nikamzuiya nguo zake, lakini akazivuta na akapanda minbar na akatoa khutbah kabla ya kuswali. Nikamwambia, 'Wallaahi nyinyi munayabadilisha mambo yalivyo'..."

KUTAMKA *TAKBEER* MWANZONI MWA KHUTBAH

Amma kuhusu kufungua khutbah kwa takbeer, hakuna riwaya iliyoswihi kutoka katika Sunnah kuhusu jambo hilo, na huu pia ndio msimamo wa Ibn al-Qayyim.'

KIKAO BAINA YA KHUTBAH MBILI

Hakuna hadeeth iliyo swaheeh ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) inayobainisha yakwamba khutbah ya 'Idd igawanywe sehemu mbili baina ya kikao kati yake.

KUSIKILIZA KHUTBAH

Kukaa baada ya swala ili kuhudhuria khutbah si jambo la waajib kama ilivyo swala, kulingana na matamshi ya 'Abdullaah Bin as-Sa'ib, "Niliwahi kuhudhuria swala ya 'Idd pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Na pindi alipomaliza swala, alisema, "*Sasa tutakuwa na khutbah, kwahivyo yoyote atakae kukaa kwa ajili ya khutbah anaweza kukaa, na yoyote atakae kuondoka anaruhusiwa kuondoka.*"

IWAPO 'IDD ITATOKEA KATIKA SIKU YA IJUMAA

Iyaas Bin Abu Ramlah ash-Shaamee amesema; "Nilimuona Abu Sufyaan akimuuliza Zayd Bin al-Arqam, 'Wewe uliwahi kuwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) pindi mojawapo ya 'Idd ilipotokea katika siku ya Ijumaa?' Akasema, 'Naam'. Akamuuliza, mukafanya nini?' Akamjibu, 'Kuliswaliwa swala ya 'Idd kasha tukaruhusiwa kutoiswali Jumu'ah, kwani alisema: "*Yoyote atakae (kuiswali Jumu'ah) na aswali.*"

Vilevile imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba 'Idd ikiangukia siku ya Ijumaa, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, "'*Idd Mbili zimekutana katika siku yenu hii, kwahiyo yoyote atakae, basi ameruhusiwa kutoiswali swala ya Ijumaa. Sisi tutaziunganisha.*"

Huu ndio mfumo wa Maswahaba (رضي الله عنهم). Imepokewa yakwambaq katika siku kama hizo, 'Ali (رضي الله عنه) alikuwa akisema, "Yoyote atakae kuziunganisha, basi aweza kufanya hivyo, na atakae kukaa nae aweza kujikalia.

MAAMKUZI YA 'IDD

Jubayr Bin Nafeer amesema, "Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikuwa wakikutana katika siku ya 'Idd baadhi yao walikuwa wakiwaambizana, *Taqabbala-Llwahu Minnaa Waminkum*. (Twamuomba Allaah atutaqabalie sisi na nyinyi).

Amesema Muhammad Bin Ziyaad, "Nilikuwa pamoja na Abu Umaamah al-Baahilee na baadhi ya Maswahaba wengine wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Walipokuwa wakirudi kutoka kwenye swala ya 'Idd, baadhi yao walikuwa wakiambizana *Taqabbala-Llwahu Minnaa Waminkum*. (Twamuomba Allaah atutaqabalie sisi na nyinyi).

Kiwango cha maamkuzi ni kama hicho kilichotajwa kuhusiana na 'Idd. Haifai kwa wale wenye kupenda kufuata Sunnah kushikilia mila nyengine za watu wa sehemu zao katika maamkuzi ya 'Idd ambayo huwa na nyongeza juu ya mila hii ya Uislamu.